JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FUNGU: 84

MKOA WA SINGIDA

MPANGO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MKOA WA SINGIDA KWA BAJETI YA MWAKA 2015/2016, 2016/17 NA MAKADIRIO YA MWAKA 2017/2018

Imeandaliwa na:

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 05
Singida.

Simu. Na. +255262502089/2249
Nukushi Na. +255262502078

2017

1.1 Utangulizi

Makadirio ya Mkoa wa Singida kwa mwaka 2017/2018 yameandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Kitaifa na kuandaa Bajeti ya Mwaka 2017/18, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo II wa Miaka 5, Mpango Mkakati wa Mkoa wa Kupunguza Umaskini na Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakati wa kupitisha bajeti ya Mkoa ya Mwaka 2016/17.

1.2 Malengo makuu ya mpango

(a) Kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa ili ziweze kufuatilia utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kutoa taarifa.

(b) Kuimarisha na kusimamia uboreshaji wa Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali za Mitaa.

(c) Kuhakikisha Serikali za Mitaa zinaendeshwa kwa misingi ya Utawala Bora.

(d) Kuhakikisha kuwepo kwa utaratibu wa sera za kisekta na programu za maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(e) Kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa wa kusimamia utekelezaji wa Sera za Kisekta pamoja na Sera zinazolenga katika kupambana na UKIMWI, Vita dhidi ya RUSHWA, Madawa ya Kulevya na uharibifu wa Mazingira.

1.3 Dira (Vision) ya Mkoa

Kuwa Sekretarieti ya Mkoa inayoongoza kuzishauri na kuwezesha juhudi za Mamlaka za Serikali za Mitaa katika shughuli za maendeleo.

1.4 Mwelekeo (Mission) ya Mkoa

Kuziwezesha na kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuleta Maendeleo endelevu ya kiuchumi na ustawi wa jamii na kuwa kiungo muhimu kati ya Wizara na Wadau wengine wa maendeleo.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2015/2016

Katika mwaka wa fedha 2015/16 Mkoa wa singida uliidhinishiwa na Bunge jumla ya Shs.145,838,200,000/=. Kati ya hizo **Shs.108,953,102,000/=** ni kwa ajili ya mishahara, **Shs.14,228,857,000**/= kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shs.22,656,241,000**/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **Shs.18,192,310,000/=** ni fedha za ndani na **Shs.4,463,931,000**/= ni fedha za nje.

Hadi tarehe 31/06/2016 Mkoa ulikwisha pokea na kutumia jumla ya Tsh. 122,927,807,850 sawa na asilimia 85 ya bajeti iliyoidhinishwa.

2.1 Maduhuli ya Mkoa na Makusanyo ya Halmashauri kwa Mwaka 2015/2016

Mkoa wa Singida katika mwaka 2015/2016 ulipangiwa kukusanya **Sh.7,643,669,575**/= na hadi Juni 2016 Mkoa ulikusanya **Sh.7,135,379,015/=** Sawa na asilimia **76.0** ya lengo la mwaka, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato ya Mkoa hadi Juni 2016

		Makadirio 2015/2016	Mapato halisi Hadi Juni 2016	Asilimia
SEKRETARIETI YA MKOA		-	-	-
HALMASHAURI:				
	Singida MC	2,986,364,000	2,480,790,038	**83.0**
	Singida DC	842,760,000	543,008,569	**64.0**
	Iramba DC	1,602,179,624	1,137,613,793	**71.0**
	Manyoni DC	1,798,366,750	1,627,283,340	**90.0**
	Mkalama Dc	986,969,200	667,400,000	**68.0**
	Ikungi Dc	1,127,030,000	679,283,275	**60.0**
Jumla Halmashauri		**9,343,669,574**	**7,135,379,015**	**76.0**
JUMLA KUU		**9,343,669,574**	**7,135,379,015**	**76.0**

2.2 Matumizi ya Kawaida ya Mwaka 2015/2016

Mkoa wa Singida kwa mwaka 2015/2016 uliidhinishiwa jumla ya **Sh.123,181,959,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Sh.108,953,102,000/=** na Matumizi Mengineyo ni **Sh.14,228,857,000/=.**

Hadi Juni, 2016 kiasi cha **Shs.112,914,599,662/=** kilipokelewa na kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri sawa na asilimia **91.7** ya fedha iliyoidhinishwa.

Muhtasari wa Matumizi hadi Juni, 2016 ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Makadirio na Matumizi ya Kawaida ya Mkoa hadi Juni, 2016

	Bajeti Iliyo idhinishwa 2015/2016	Fedha Zilizo-Pokelewa Hadi Juni, 2016	Matumizi Hadi Juni, 2016	% ya Matumizi kwa Fedha Iliyoidhinishwa
Sekretarieti ya Mkoa				
Mishahara	8,623,503,000	6,238,918,100	6,238,918,100	**72.3**
Matumizi Mengineyo	1,345,047,000	931,688,940	931,679,142	**69.3**
Jumla	**9,968,550,000**	**7,170,607,040**	**7,170,597,242**	**71.9**
Halmashauri				
Mishahara	100,329,599,000	97,409,257,680	97,409,257,680	**97.1**
Matumizi Mengineyo	12,883,810,000	8,334,734,942	8,334,734,942	**64.7**
Jumla	**113,213,409,000**	**105,743,992,622**	**105,743,992,622**	**93.4**
Jumla Kuu	**123,181,959,000**	**112,914,599,662**	**112,914,589,864**	**91.7**

Orodha ya Shughuli Muhimu Zilizotekelezwa

Orodha ya shughuli muhimu zilizotekelezwa kwa upande wa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ni pamoja na:

- Kuendesha shughuli za Ofisi za kila siku ambazo ni pamoja na kulipia gharama za simu, umeme na maji

- Kuendesha vikao vya kisheria ikiwa ni pamoja na Kamati ya Ushauri ya Mkoa, Kamati Maalum ya Ajira, Kamati ya Ulinzi na Usalama na Bodi za Ajira za Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Sekretarieti ya Mkoa ilifanya ufuatiliaji na tathimini ya shughuli zinazotekelezwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kutoa ushauri

- Kutengeneza na kuhudumia magari, kununua vifaa vya ofisi na samani.

- Kuajiri watumishi wapya wa kada za afya na walimu wa shule za msingi na sekondari

- Kuratibu shughuli za kilimo na mifugo katika Serikali za Mitaa na kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji ili kuongeza tija katika uzalishaji.

- Kujenga na kukarabati barabara za Wilaya na Vijiji ili kuwezesha wakulima kufikisha mazao yao katika masoko.

- Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru ndani ya Mkoa.

- Kuandaa na kuratibu ziara za Viongozi wa kitaifa Mkoani

- Kufuatilia na kusimamia ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,

- Kufuatilia na kukagua miradi ya Maendeleo katika Halmashauri.

- Kuendelea kutoa elimu kuhusu namna ya kujikinga na virusi vya UKIMWI katika maeneo ya kazi.

- Kuratibu shughuli za mgambo.

2.3 Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2015/2016

Katika mwaka 2015/2016 Mkoa uliidhinishiwa jumla ya **Sh.22,656,241,000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Sh.18,192,310,000/=** ni Fedha za Ndani na **Sh.4,463,931,000/=** ni Fedha za Nje.

Hadi kufikia Juni, 2016 jumla ya **Sh.10,013,404,588/=** zilipokelewa sawa na asilimia **44.2** ambapo zote zimetumika sawa na asilimia 100 ya fedha zilizopokelewa kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3.

Jedwali Na. 3: Makadirio na Matumizi ya Fedha za Maendeleo hadi Juni, 2016

	Bajeti Yaliyoidhinishwa 2015/2016	Fedha Zilizopokelewa hadi Juni, 2016	Matumizi Hadi Juni, 2015	% ya Matumizi Kwa Fedha Iliyoidhinishwa
Sekretarieti ya Mkoa				
Fedha za Ndani	3,970,154,000	-		-
Fedha za Nje	115,058,000	342,178,155	342,178,125	**297.4**
Jumla	**4,085,212,000**	**342,178,155**	**342,178,125**	**8.4**
Halmashauri				
Fedha za Ndani	14,222,156,000	9,308,817,433	9,308,817,433	**65.5**
Fedha za Nje	4,348,873,000	362,409,000	362,409,000	**8.3**
Jumla	**18,571,029,000**	**9,671,226,433**	**9,671,226,433**	**52.1**
Jumla Kuu	**22,656,241,000**	**10,013,404,588**	**10,013,404,558**	**44.2**

Orodha ya Shughuli Muhimu zilizotekelezwa

Orodha ya shughuli muhimu zilizotekelezwa kwa upande wa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ni pamoja na:

- Ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu za Kilimo (DADS), Maji (RWSSP), Programu ya Kuboresha Sekta ya Afya (HSBF), Programu ya Kudhibiti UKIMWI na Programu ya Kuendeleza Elimu ya Sekondari (SEDP) ulifanywa katika Halmashauri.

- Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Programu ya Maji (RWSSP), Programu ya Kuboresha Sekta ya Afya (HSBF), Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri (LGCDG), Programu ya Kuendeleza Elimu ya Sekondari (SEDP), Mradi wa Kudhibiti UKIMWI na Virusi vya UKIMWI, Mpango wa Pamoja wa Kuboresha Sekta ya Afya (HSBF) Miradi inayotumia fedha za ndani iliendelea kutekelezwa. Kazi muhimu zilizofanywa ni pamoja na:-

  - ✓ Skimu mbali mbali za umwagiliaji ziliendelea kutekelezwa katika Halmashauri.

  - ✓ Ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya, zahanati na nyumba za watumishi wa afya ulifanyika.

  - ✓ Ununuzi na usambazaji wa madawa na vifaa tiba kwenye vituo vya tiba ulifanyika.

  - ✓ Huduma za afya ikijumuisha tiba na chanjo zilitolewa katika Halmashauri.

  - ✓ Ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msing na Sekondari ikiwa ni pamoja na madarasa, vyoo, mabweni, hosteli, majengo ya Utawala, maabara na nyumba za walimu uliendelea kufanyika.

  - ✓ Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na visima virefu, matanki ya kuhifadhia maji ulifanyika.

  - ✓ Ujenzi wa barabara na matengenezo ya barabara za kawaida, muda maalum, sehemu korofi na madaraja ulifanyika.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/2017

Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mkoa wa Singida uliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi. **161,715,919,000.** Kati ya hizo Tshs. **112,860,815,000** ni kwa ajili ya mishahara, Tshs. **10,541,470,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tshs. **32,921,097,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo Tshs. **20,354,577,000** ni fedha za ndani na Tshs. **12,566,520,000** ni fedha za nje. Mchanganuo wa utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ni kama ufuatavyo:

3.1 Mapato ya Mwaka 2016/2017

Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika maeneo yasiyo ya ruzuku (own source) kwa Mwaka 2016/2017 zilikadiriwa kukusanya jumla ya **Sh.11,345,781,448/=.** Hadi kufikia Machi, 2017, kiasi cha **Sh.3,898,857,846**/= kilikusanywa sawa na asilimia **34.4** ya lengo la mwaka, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Makusanyo ya Mapato ya Mkoa hadi Machi 2017

		Makadirio 2016/2017	Mapato Hadi Machi 2017	Asilimia
SEKRETARIETI YA MKOA		**-**	**-**	**-**
HALMASHAURI:				
	Singida MC	3,269,845,240	836,826,738	25.6
	Singida DC	1,014,101,746	443,253,631	43.7
	Iramba DC	1,927,751,587	663,097,002	34.4
	Manyoni DC	1,760,499,700	719,513,560	40.9
	Mkalama Dc	940,000,000	498,337,830	53.0
	Ikungi Dc	1,080,000,000	406,375,096	37.6
	Itigi Dc	1,353,583,175	331,453,989	24.5
Jumla Halmashauri		**11,345,781,448**	**3,898,857,846**	**34.4**
JUMLA KUU		**11,345,781,448**	**3,898,857,846**	**34.4**

Baadhi ya Halmashauri zimekusanya chini ya 50% ya lengo kwa kuwa chanzo kikuu cha mapato ni ushuru wa mazao ambao kwa sasa haujaanza kutozwa.

3.2 Matumizi ya Kawaida ya Mwaka 2016/2017

Mkoa kwa mwaka 2016/2017 uliidhinishiwa jumla ya **Sh. 130,362,392,236/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara ni **Sh.112,860,815,000/=** na Matumizi Mengineyo **ni Sh. 17,501,577,236/=).**

Hadi Machi, 2017 kiasi cha **Sh.76,645,494,740/=** kilipokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ambapo kiasi chote cha **Sh.76,645,494,740/=** kilitumika sawa na asilimia **59** ya fedha iliyoidhinishwa. Muhtasari wa Matumizi hadi Machi, 2017 ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Makadirio na Matumizi ya Kawaida ya Mkoa hadi Machi, 2017

	Bajeti Iliyo idhinishwa 2016/2017	**Fedha Zilizo-Pokelewa Hadi Machi, 2017**	**Matumizi Hadi Machi, 2017**	**% ya Matumizi kwa Fedha Iliyoidhinishwa**
Sekretarieti ya Mkoa				
Mishahara	6,386,408,000	4,092,416,200	4,092,416,200	**64**
Matumizi Mengineyo	3,055,135,236	1,835,699,213	1,835,699,213	**60**
Jumla	**9,441,543,236**	**5,928,115,413**	**5,928,115,413**	**63**
Halmashauri				
Mishahara	106,474,407,000	63,750,686,500	63,750,686,500	**60**
Matumizi Mengineyo	14,446,442,000	6,966,692,827	6,966,692,827	**48**
Jumla	**120,920,849,000**	**70,717,379,327**	**70,717,379,327**	**58**
Jumla Kubwa	**130,362,392,236**	**76,645,494,740**	**76,645,494,740**	**59**

Orodha ya Shughuli Muhimu zilizotekelezwa

Orodha ya shughuli muhimu zilizotekelezwa kwa upande wa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ni pamoja na:

- Ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo Wilayani ulifanywa na wananchi walihimizwa kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao ikiwa ni pamoja na utenenezaji wa Madawati, ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa nyumba za walimu na ujenzi wa Maabara katika shule za Sekondari za Serikali.

- Kikao kimoja cha kisheria (Kamati ya Ushauri ya Mkoa) kilifanyika

- Vikao 2 vya Kamati ya Mapato na Matumizi vilifanywa kujadili hali ya utekelezaji wa Bajeti ya Mkoa kwa robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2016/2017.

- Ushauri wa kitaalamu juu ya utekelezaji wa shughuli za sekta za Kilimo, Mifugo, Ushirika, Maendeleo ya Jamii, Afya na Barabara ulitolewa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wadau wengine.

- Ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa Programu za Maendeleo zinazofanywa wilayani ulifanyika.

- Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfumo wa ukusanyaji wa Mapato ulifanyika.

- Huduma za tiba katika Hospitali ya Mkoa zilitolewa kwa wananchi.

- Uandikishaji wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari ulifuatiliwa na usimamizi wa mitihani ya Shule za Msingi na Sekondari ulifanyika.

- Maandalizi ya Mpango Kazi wa Mwaka 2017/2018 na Mipango na Bajeti ya Mwaka 2017/2018 yanaendelea kufanyika.

3.3 Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017

Katika mwaka 2016/2017 Mkoa ulitengewa jumla ya **Sh.32,921,097,000**/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Sh.20,354,577,000/=** ni Fedha za Ndani na **Sh.12,566,520,000/=** ni Fedha za Nje.

Hadi kufikia Machi 2017 jumla ya **Sh.12,650,949,945/=** zilipokelewa sawa na asilimia **32** ambapo **Sh.10,622,097,900/=** zimetumika na nyingine zipo kwenye miadi (commitments). Makadirio na Matumizi ya Fedha za Maendeleo hadi Machi 2017 ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 6: Makadirio na Matumizi ya Fedha za Maendeleo hadi Machi 2017

	Bajeti Iliyo idhinishwa 2016/2017	Fedha Zilizo-Pokelewa Hadi Machi, 2017	Matumizi Hadi Machi, 2017	% ya Matumizi Kwa Fedha Iliyoidhinishwa
Sekretarieti ya Mkoa				
Fedha za Ndani	3,250,000,000	2,345,000,000	366,351,818	**11.3**
Fedha za Nje	170,843,000	142,810,000	92,606,136	**54.2**
Jumla	**3,420,843,000**	**2,487,810,000**	**458,957,954**	**13.4**
Halmashauri				
Fedha za Ndani	17,104,577,000	4,080,792,000	4,080,792,000	**23.9**
Fedha za Nje	12,395,677,000	6,082,347,945	6,082,347,945	**49.1**
Jumla	**29,500,254,000**	**10,163,139,945**	**10,163,139,945**	**34.5**
Jumla Kubwa	**32,921,097,000**	**12,650,949,945**	**10,622,097,900**	**32.3**

Mchanganuo wa makadirio, matumizi na hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri za Wilaya na Manispaa ni kama unavyooneshwa hapa chini.

3.4 Miradi ya Sekretarieti ya Mkoa kwa Mwaka 2016/2017

Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Sekretarieti ya Mkoa hadi Machi, 2017 jumla ya **Sh. 2,429,951,000/=** sawa na asilimia **72.7** zilikuwa zimetolewa na kiasi kilichotumika ni asilimia 13.4 ya fedha iliyotolewa kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 7 hapo chini:

Jedwali Na.7: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Sekretarieti ya Mkoa hadi Machi, 2016

Namba ya Mradi	Jina la Mradi	Jumla ya fedha zote	Fedha zilizotolewa
6338	Ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya	800,000,000	720,000,000
6332	Mfuko wa miradi ya kujitegemea	45,000,000	45,000,000
6339	Ukarabati wa nyumba za Serikali	520,000,000	520,000,000
5499	Mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI (HIV/AIDS)	56,400,000	-
6531	Uratibu na Usimamizi wa Miradi	40,000,000	40,000,000 -
4404	Mipango ya Wilaya ya Maendeleo ya Kilimo (DADPS)	8,000,000	-
4390	Mfuko wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari	20,000,000	-
3280	Progamu ya Usambazaji wa Maji Vijijini	37,575,000	25,000,000
5486	Mpango wa Uboreshaji wa Sekta ya Afya	133,268,000	99,951,000
5402	Ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa	1,760,600,000	1,020,000,000
Jumla Kuu		**3,420,843,000**	**2,429,951,000**

3.5 Miradi ya Halmashauri kwa Mwaka 2016/2017

Miradi inayosimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2016/2017 iliidhinishiwa jumla ya sh.29,500,254,000/= Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya sh.10,163,139,945/= zikiwa zimetolewa, sawa na asilimia 34.5 ya fedha zilizoidhinishwa.

4.0 CHANGAMOTO KUBWA ZA UTEKELEZAJI ZILIZOJITOKEZA

Changamoto kubwa zinazoathiri utekelezaji wa Bajeti ya Mkoa na Halmashauri ni pamoja na:-

- Uhaba wa vitendea kazi hasa magari ya viongozi Wakuu wa Mkoa, baadhi ya Wakuu wa Wilaya na ya Wakurugenzi.
- Kukosekana kwa fedha za kukidhi gharama za uhamisho wa watumishi hususan katika Wilaya mpya na Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa.

- Kukosekana kwa fedha za kukidhi posho za Maofisa wanaokaimu nafasi mbalimbali ambao hawajapata kibali cha Katibu Mkuu - Utumishi.
- Kuongezeka kwa gharama za usimamizi kutokana na kuongezeka Wilaya na Halmashauri.
- Magari ya kufanyia kazi ya ufuatiliaji na ukusanyaji wa mapato kwa Halmashauri (utawala, fedha, Afya, Elimu)
- Madeni ya Watumishi na wazabuni (kukaimu, uhamisho, likizo)
- Kutotolewa kwa Fedha za *on-call* kwa kipindi chote toka mwaka wa fedha uanze.

5.0 MAWASILISHO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

5.1 Makadirio ya mapato kwa mwaka 2017/2018

Makadirio ya Mapato kwa mwaka 2017/2018 kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri kwa maeneo yasiyo ya ruzuku (own source) ni kama ilivyo katika Jedwali Na.8.

Jedwali Na. 8: Makadirio ya Mapato ya Mkoa kwa Mwaka 2017/2018

HALMASHAURI:		**Makadirio 2017/18**	**Fedha za Maendeleo (60%)**	**Fedha za matumizi ya Kawaida (40%)**
	Singida MC	3,312,625,000	1,987,575,000	1,325,050,000
	Singida DC	2,157,244,000	1,600,293,000	556,951,000
	Iramba DC	1,920,812,000	1,152,487,000	768,325,000
	Manyoni DC	2,488,727,000	1,493,236,000	995,491,000
	Ikungi DC	1,446,793,000	868,076,000	578,717,000
	Mkalama DC	1,043,005,000	625,803,000	417,202,000
	Itigi DC	1,902,289,000	835,427,000	1,066,862,000
JUMLA KUU		**14,271,495,000**	**8,562,897,000**	**5,708,598,000**

5.2 MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mkoa umekadiria kutumia **Sh.167,482,840,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh.14,271,495,000/=** ni makusanyo ya ndani, Mishahara ni **Sh.140,332,780,000/=** na Matumizi Mengineyo (OC) ni **Sh.12,878,565,000/=.** Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halamshauri ni kama ifuatavyo:

5.2.1 SEKRETARIATI YA MKOA

Jumla ya Sh**. 12,243,811,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi Maendeleo ya Sekretariati ya Mkoa. Kati ya fedha hizo Sh. **7,067,402,000** ni Mishahara na Sh. **1,572,740,000** ni Matumizi Mengineyo na **3,603,669,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 9 hapa chini.

Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida ya Sekretarieti ya Mkoa

KIFUNGU	JINA LA KIFUNGU	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	MAENDELO	JUMLA
1001	Utawala na Utumishi	262,597,000	553,038,000	1,615,000,000	2,351,297,000
1002	Fedha na Uhasibu	28,080,000	131,751,600	0	159,831,600
1003	Ukaguzi wa Ndani	28,080,000	59,490,000	0	87,570,000
1004	Manunuzi	6,000,000	54,180,000	0	60,180,000
1005	DAS - Singida	55,840,000	231,199,200	0	287,039,200
1006	DAS - Manyoni	55,840,000	280,207,200	0	336,047,200
1007	DAS - Iramba	55,840,000	237,990,000	0	293,830,000
1008	DAS - Ikungi	63,040,000	254,610,000	0	317,650,000
1009	DAS - Mkalama	63,040,000	256,839,000	0	319,879,000
1014	DAS - Sheria	10,000,000	23,004,000	0	33,004,000
1015	Habari na Mawasiliano	9,500,000	22,719,000	0	32,219,000
2001	Mipango na Uratibu	67,880,000	124,320,000	96,400,000	288,600,000
2002	Uchumi na Uzalishaji	29,080,000	273,318,000	8,000,000	310,398,000
2003	Miundombinu	33,980,000	190,209,000	0	224,189,000
2004	Ustawi wa Jamii	29,080,000	161,288,000	0	190,368,000
2005	Serikali za Mitaa	29,080,000	129,270,000	140,000,000	298,350,000
2006	Sekta ya Elimu	285,663,000	178,962,000	20,000,000	484,625,000
2007	Sekta ya Maji	29,080,000	98,106,000	37,575,000	164,761,000
3001	Hospitali ya Mkoa	431,040,000	4,760,669,000	1,686,694,000	6,878,403,000
3002	Afya kinga	0	26,772,000	0	26,772,000
Jumla		**1,572,740,000**	**7,067,402,000**	**3,603,669,000**	**12,243,811,000**

5.2.2 SERIKALI ZA MITAA

Katika Mwaka wa 2017/2018 Bajeti za Matumizi ya Kawaida kwa Serikali za Mitaa zinajumuisha Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Fedha zinazokusanywa kutokana na vyanzo vyao (own sources).

Matumizi ya Kawaida kwa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2017/2018 yamekadiriwa kuwa **Sh.157,941,496,000/=.** Kati ya fedha hizo **Sh.143,670,001,000/=** ni ruzuku kutoka Serikali kuu na **Sh.14,271,495,000/=** ni makusanyo ya ndani. Kiasi cha **Sh.132,284,838,000/=** kinaombwa kwa ajili ya Mishahara na **Sh.11,385,163,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Mgawanyo wa Makadirio hayo kwa kila Halmashauri ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 10.

Jedwali Na. 10: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa kila Halmashauri

Halmashauri	Matumizi Mengineyo	Mishahara	Jumla
Singida MC	1,646,417,000	21,082,753,182	26,041,795,182
Singida DC	1,601,363,000	20,849,542,000	24,608,149,000
Iramba DC	1,503,627,000	21,343,517,866	24,767,956,866
Manyoni DC	2,373,301,000	20,623,147,800	25,485,175,800
Mkalama Dc	1,440,388,000	13,798,839,964	16,282,232,964
Ikungi Dc	1,076,867,000	18,320,609,984	20,844,269,984
Itigi Dc	1,743,200,000	16,266,427,204	19,911,916,204
Jumla Halmashauri	**11,385,163,000**	**132,284,838,000**	**157,941,496,000**